**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule:0765346576**

**Makamu Mkuu wa Shule:0755227725/0762003884**

**Mwl wa bweni: 0758739885**

**Shule ya Sekondari: BINZA**

**S.L.P: 319 - MASWA**

**Tarehe: 19 / 04/ 2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BINZA HALMASHAURI YA MASWA MKOA SIMIYU MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari **BINZA** ipo umbali wa Kilometa mbili (02) Mashariki mwa Mji wa Maswa. Usafiri wa pikipiki kutoka maswa stendi ni shilingi elfu mbili tu ( Tsh 2000/=). Muhula wa Masomo unaanza tarehe ................ hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe...................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**



CS CamScanner

**2.Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali rangi ya ugoro mbili (2) zenye marinda mawili kila upande **isiwe model** kwa ajili ya darasani;
ii. Mashati mikono mirefu mawili (2) kwa ajili ya darasani.
iii. Sare ya Michezo ni tracksuit ya dark bluu, Bukta 1 na t-shirt ya bluu na raba rangi yoyote.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta rangi ya ugoro.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali ya kaki moja au zaidi, T-shirt rangi ya **dark bluu** yenye kola ya kaki ikiwa na nembo ya shule mgongoni.
ix. Tai ugoro ndefu mbili (2) .

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari ya kutosha (counter book quire 3) kulingana na idadi ya masomo katika mchepuo aliopangwa.;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
**vi.** Godoro lipo shuleni na linakodishwa kwa gharama ya Sh. 10,000/= kwa mwaka hivyo mwanafunzi **haruhusiwi** kuja na godoro bali alipie fedha hiyo kwenye akaunti no. **30802500325 NMB, JINA LA AKAUNTI;- ELIMU YA KIJITEGEMEA BINZA SEKONDARI.**
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari, foronya ya godoro 1 rangi ya bluu bahari, na chandarua 1;
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1(na mpini wake), brashi ngumu ya chooni 1, mfagio wa ndani 1, chelewa 1 na mopa 1.

**2.3 Michango mbalimbali**

**Shule ya Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

NB: Michango yote iwekwe kwenye akaunti ya shule kwa jina la **BINZA SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION ACCONT – 30801100004 benki NMB.** mwanafunzi asije na pesa shuleni haitapokolewa, Aje na risiti ya malipo hayo ikiwa imeandikwa jina la mwanafunzi.

3. **Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi**

**kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na



CamScanner

iv. Picha mbili (2) passport size za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Mimi ………………………………………………Kidato cha ……… Baada ya kusoma kwa makini na kuelewa sheria za shule na ahadi za mwanafunzi zilizowekwa Na Uongozi wa shule. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu pamoja na Mkuu wa Shule kuwa nitazitii; kuzingatia; kutekeleza na kufuata sheria zote za shule na kwamba nikizivunja sheria za shule nijihesabu nimejifuta shule mwenyewe.

Jina kamili na sahihi ya mwanafunzi……………………………….……Tarehe………………… Jina kamili na sahihi ya Mzazi/mlezi wangu…………….…………..………………… Tarehe……… Namba ya simu ya mzazi/mlezi …………………………

Taja jina la mtu wa karibu ambaye shule inaweza kuwasiliana nae kwa jambo lolote iwapo mzazi/mlezi akikosekana..………………………………Anwani……….. namba yake ya simu………………………

Jina na sahihi ya Mkuu wa Shule **AMEDE M. NDONJE** ,…………….. Tarehe 19.4.2020

THE HEADMASTER
BINZA SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 319
MASWA-SIMIYU



CamScanner

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART 'A'

TO THE MEDICAL OFFICER

..................................

....................................

FROM

............................

.............................

Mr..............................................................(Name in full)

Please examine the above named as to his physical and mental fitness for a full – time student. The examination should include the following categories (I – III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect

I (a) Eyesight

(b) Hearing

(c) Speech

(d) Limbs

(e) Venereal Diseases

(f) Leprosy

(g) Epilepsy

(h) TB

II Neuroses

III Other serious diseases

Date.........................................Signature...................................

## PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)



CamScanner

I have examined the above – named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I (a) Eyesight......................

(b) Hearing.......................

(c) Speech.......................

(d) Limbs........................

(e) Venereal Diseases...................

(f) Leprosy...............................

(g) TB .......................................

II Neuroses........................................................................................

III Other serious diseases ...........................................................................

Date............................................Signature....................................

Station........................................ Designation...............................

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

## ORODHA YA VITABU

### 1. HISTORY

1. ADVANCED LEARNER'S HISTORY 5 & 6 - OXFORD
2. MASTERING HISTORY CARTER - CARTER
3. HISTORY FOR ADVANCED LEVEL - ZISTI KAMILI

### 2. GEOGRAPHY

1. PHYSICAL GEOGRAPHY - MSABILA
2. HUMAN ECONOMIC GEOGRAPHY - MSABILA
3. PHYSICAL GEOGRAPHY - MONK HOUSE
4. PHYSICAL GEOGRAPHY - BUNNET
5. INTERGRATED GEOGRAPHY - DAVID WAUGH



CS CamScanner

### 3. ENGLISH LANGUAGE

1. ADVANCED ENGLISH LANGUAGE - OXFORD
2. ENGLISH LANGUAGE - NICHOLAUS ASHEL
3. LITERATURE IN ENGLISH -
4. ENGLISH LITERATURE BOOKS
   - Rwanda Magere
   - His Excellence The Head of States
   - I will marry when I want
   - Betrayal in the City
   - Devine Province
   - A man of the People
   - The beautiful Ones are not yet born

### 4. PHYSICS

1. PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XI (S. CHAND'S)
2. PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XII (S. CHAND'S)
3. ADVANCED LEVEL PHYSICS 7$^{TH}$ EDITION (MICHAEL NELKON)
4. ADVANCED PHYSICS (LOGER MANKASTER)

### 5. BIOLOGY

1. BIOLOGICAL SCIENCE FOR ADVANCED LEVEL 02$^{nd}$ or 03$^{rd}$ Edition
2. UNDERSTANDING BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL

### 6. CHEMISTRY

1. CONCEPTUAL CHEMISTRY - CHAND VOL. XI, XII
2. RAMSDEN - 04$^{TH}$ Edition
3. TANZANIA INSTUTE OF EDUCATION BOOKS

### 7. ADVANCED MATHEMATICS

1. PURE MATHEMATICS 1 & 2 - AUTHOR BACKHOUSE
2. ADVANCED LEVEL MATHEMATICS - C.J TRANTER
3. ADVANCED LEVEL MATHEMATICS - CHAND
4. ENGINEERING MATHEMATICS -
5. CONSCISE MATHEMATICS - BOSTOCK & CHANDLER



CamScanner